KUELEKEA TEOLOJIA YA WASALVATORIANI KUHUSU WOKOVU

01 Januari 2015

Fr. Thomas Perrin SDS,

UTANGULIZI

Mtakatifu Agustino aliandika "Wewe, Mungu Baba, unatuhamasisha kupata furaha tunapokusifu, kwa sababu umetuumba tukutafute na, kwa hiyo, mioyo yetu haiwezi kupumzika mpaka itakapopumzika katika Wewe."[i] Sentensi hii inafupisha tauhidi tajiri inayohusu hasa 'wokovu.' Kwa maana pana, viumbe vile alivyoviumba Mungu Baba nje ya nafsi yake vitarudi kwake Baba na 'kupumzika' ndani ya Baba tena baada ya safari ile nje ya Baba. Huu ulikuwa mpango wa Mungu Baba hata kabla ya kuumba viumbe kutoka kuumbwa na kurudi baada ya muda hapa duniani. Tunaweza kuelewa maana ya neno 'wokovu' kwa namna mbili:

1) Mchakato unaotumiwa na Mungu Baba kutekeleza mpango wake kama …mpango ambao angeutimiliza wakati utimiapo…kukusanya pamoja viumbe vyote, kila kitu mbinguni na duniani, chini ya Kristo."[ii]

2) Kama matokeo ya mwisho ya mchakato ule, yaani, uhai wa milele katika Mungu Baba.

Yesu, Mwokozi wetu, na Roho Mtakatifu wamefunua mpango wa Mungu Baba kwa wokovu na wameshaanza kutekeleza kwa nguvu mchakato ule wa Baba katika historia ya wanadamu. Wanavyotushirikisha katika mchakato huu, sisi wanadamu wenye uwezo wa kumtambua Mungu Baba na kazi ya Baba kati yetu na ndani yetu, tunaitwa si kuunda tu "uhusiano wa kijamii wa teknolojia na utamaduni" lakini pia "kufikia umoja kamili katika Yesu Kristo"[iii]. (Lumen Gentium I.1) Hapo tutakapoogelea katika upendo wa Mungu Baba, kila chozi litaondolewa. (Isaya 25.8), na tutamsifu Mungu Baba bila mwisho (Ufunuo 5.13): Baba, atakayetawala "juu ya vyote" (1 Cor 15.28) ((au: Baba "awe yote katika wote" (utafsiri wa zamani))).

KUELEKEA TEOLOJIA YA WASALVATORIANI KUHUSU WOKOVU

Tunajiuliza: sisi SDS, je, tutatazama Tauhidi ya Wokovu vipi? Kwanza, tutaje baadhi ya mada kuu muhimu: Kwanza, tukitaka kuwa "mitume" duniani, inatubidi kuwa na upendo na uhusiano wa karibu sana na Mungu Baba sisi wenyewe. La sivyo, tutakapo jaribu kuongoza wengine tutakuwa pofu tunaoongoza pofu wenzetu! Mara nyingi tunaeleza 'uhusiano huu wa karibu sana' kama hali ya kumtambua Mungu Baba.

"Pamoja na Maria, Mama yake, tunampeleka kwa wengine mwokozi ambaye tumemjua sisi wenyewe."
Sheria # 10

Halafu, Baba anatuita kushirikiana naye, kushirikiana na sisi wenyewe na kwa watu wengine katika mchakato wa wokovu. Tunatafuta, si wokovu wetu binafsi tu, lakini pia wokovu wa wote. Hatutapumzika – hata kwa dakika moja! – kama bado kuna mtu mmoja duniani ambaye hamfahamu na hampendi Mungu Baba zaidi kuliko watu wote na vitu vyote.[iv] (Sheria ya Familia ya Kisalvatorian), Utangulizi, mstari wa kwanza.) Kumjua Mungu Baba na kumpenda ni shabaha ya Tauhidi ya Wokovu. Sisi SDS tumeitwa kuwa watumishi wa Tumaini kwa watu wanaohitaji mwongozo, wanaohitaji nguvu na wanaohitaji uhusiano wa mapendo na Mungu wao anaotafuta wokovu wao. Tunajaribu "kuongoza wengine wapate ukamilifu" tunapotambua kwamba sababu za maumivu ya wenzetu mara nyingi ni nje au juu ya uwezo wao. Mara nyingi ni

dhambi za wengine – au walau kutokujua njia za uadilifu – zinazosababisha maumivu rohoni. Tunajaribu kuwasaidia wenzetu wapate uhuru – haidhuru kama wametekwa nyara na kamba za kiroho, kimwili, kiakili, kijamii au kifamilia. Tunaunga mkono na Mungu Baba anapowapa wenzetu uhuru kutoka utumwa wa mwili na wa dhambi (shetani), au katika roho au katika mwili, au kamba za zamani sana, au za karibuni zaidi. Kujaribu kumsaidia Mungu Baba kuwapa uhuru ni sehemu ya wito wetu. Mwishoni – au juu ya yote –kuwasaidia watu wote na mahali popote, wautambue Utatu Mtakatifu wa Mungu, wapende Nafsi tatu za Mungu mmoja, watumikie Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu na wote wafaulu kukaribishwa katika umoja wa Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu – haya yote ni kazi zetu sisi SDS – kutoka mwanzo wa ukandidati mpaka vifo vyetu. Tunashughulikia pia kwa maisha yetu yote katika kazi ya kuunganisha wenzetu wote katika utume wetu: sisi sote tunahudumia wote kama ndugu na dada zetu kama Yesu alivyotuonesha.

KUMJUA MUNGU

Hakuna Teolojia ya wokovu kwa wasalvatoriani ambayo itakamilika bila kufikiria msemo huu "kumjua Mungu." Muono wa haraka wa sheria ya maisha, katiba na sheria za jumla za shirika la masista wa Mungu Mwokozi,[v] kwa mfano, yaliacha mambo yafuatayo: tumaini halisi kwamba wote wamjue Mungu na Yesu Kristo ambaye Mungu alimtuma inaonekana mara nne (4). Hii inaonyesha uaminifu wa marudio ya Yn 17:3 "Uzima wa milele ndio huu, kwamba wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na yule ambaye ulimtuma, Yesu Kristo. "Katiba pia inaonyesha utume wa kumfanya Mungu, au Yesu, au "yeye" ajulikane zaidi ya mara tisa (9). Kwa ujumla, hii inaonyesha msisitizo mkubwa wa sehemu hii moja ya karama yetu. Ngoja tuitazame!

Katiba namba 4, inatufahamisha: "Yesu, kama mwokozi wa ulimwengu, ni lengo na chanzo cha maisha yetu. Kutoka kwake tunajifunza kuwa na kiu kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kama waanzilishi wetu walivyofanya. Tamaa yetu ya kuwa wake bila kujibakiza na kushiriki katika kazi yake ya wokovu inatusaidia kumjua yeye kwa karibu na kumpenda na kumtumikia bila kujibakiza na kushiriki katika kazi yake ya kumtumikia bila kujibakiza." Kiteolojia, Mungu, ambaye alitupenda kwanza, alitupa zawadi ya kumpenda yeye! Mungu anatuleta katika Umungu wake halisi kwa njia ya kirafiki kwa kutualika "kumjua" yeye, na halafu, kumpenda na kumtumikia yeye. Tunapomjua Mungu kwa moyo zaidi, tutampenda yeye zaidi na zaidi kutimiza mapenzi ya Mungu, kwa kumtumikia yeye na wengine kwa moyo wote, kutii amri za Mungu, kumsifu na kumtukuza Mungu, N.K.

Katiba namba 20, inatanguliza kumjua Mungu, na kuchukua maarifa na upendo wa Mungu katika hatua inayofuata: "… Tukijitahidi kuwa makini sana kwa royo yake (Mungu) ya kubadilisha, tunafunguliwa upendo mkuu wa Mungu na tunaendelea kuwa huru kuwapenda wote kama Kristo alivyotupenda sisi. Uwepo wake ndani yetu unatuakisia amani na furaha na kutuwezesha kuutangaza wema wake na upendo wake wa kuokoa kila mmoja ambaye amemweka katika njia yetu." Hapa, tunagundua kwamba "kumjua" Mungu kwa hakika hakutajwi, bali matunda ya ufahamu huo yanatajwa! Roho wa Mungu anafanya kazi ndani ya mazingira ya uhuru wa kila mmoja kwa kumsaidia kuweza kuwa wazi zaidi, na kuwa huru kuwaangazia wengine upendo ambao unafahamika. Mtu anaweza kusema kwamba katiba ya shirika inajadili kumjua Mungu ni kama utaratibu mpana unaotumika kwa ajili ya ukomavu wa kitume. Nikinukuu Mzaburi, utaratibu huu wa ukomavu upo pale ambapo upendo na uwajibikaji vinapokutana, tafakari na utume vinapobusiana (Angalia Zab 85:11).

Mazungumzo ya Yohana 10 yanaonyesha kuwa msaada hapa. Mwandishi wa Yohana kila wakati anakuwa na msimamo katika matumizi yake ya mada kuu za maneno. Mwandishi wa Yohana huwa anatumia vitenzi mbalimbali kwa "kujua" na wataalamu wengi wanaamini kwamba vitenzi hivi huwa vinaweza kutumika kwa kubadilishana. Lakini, mwandishi huyu anaonyesha ya kwamba vitenzi hivi huwa vinaweza kutumika kwa kubadilishana. Lakini, mwandishi huyu anaonyesha kwamba matumizi yote ya neno hili si sawa. Yohana 17:3 imetumia kitenzi "ginoskein" ambayo ni kitenzi jina ya kitenzi ya jambo linalotokea katika sentensi ile. Kila mara, katika yohana, jambo hili linaonyesha juu ya mtu anayemfahamu mtu mwingine zaidi ya vitenzi vingine, ambavyo mara nyingi inaashiria: "kupata wazo." Labda maana kubwa ya matumizi ya "ginoskein" inatoka katika yohana 10: mwokozi mwenyewe anatamka yafuatayo "Mimi ni Mchungaji Mwema, na huwajua [kondoo wangu] na walio wangu hunijua mimi, kama vile baba anijuavyo mimi na mimi humjua Baba…"

Hayo ni matumizi manne ya "ginoskein" katika sentensi moja! Lakini ina maana pana kiteolojia, kwa kuwa inalinganisha ufahamu wetu wa kibinadamu na ule wa Mungu. Kuna "ufanano" kati ya ufahamu wetu wa kibinadamu na ule wa Mungu!

Zaidi ya hayo, ufahamu wa mchungaji juu ya kondoo wake utaishia kujitoa uhai wake kwa ajili ya kondoo. (10:11) kujua na kupenda kwa asili ni kitu kimoja. Na kujua kondoo wake ni kitu cha nafsi, anajua kila mmoja kwa jina lake, anawaita na wao wanamfuata (10:3-4) kama "ufahamu" wa mwokozi juu ya kondoo wake ni upendo mpaka kujitoa uhai, nafsi (kwa jina), na kwa uhusiano (wanasikia na kufuata sauti yake), kwa hiyo ni ukweli kwamba ni upendo wenye hali ya kujitoa kwa moyo. Hili ndilo fundisho kuu tunalotakiwa kujifunza kutoka kwa mwandishi wa Yohani.

UZIMA KATIKA UKAMILIFU WAKE WOTE

Sheria zetu za familia ya Kisalvatoriani zinatukumbusha juu ya wito wetu, kufanya kazi mpaka watu wote, mahali pote, "wafahamu utajiri wa uzima kupitiaYesu Mwokozi."[vi] (Sheria, kipengele 1. No. 1)

Kwa kusema hayo, tunaweka karama yetu kwa dhati kwa maana mbili za wokovu. Tunapowaleta wengine katika utimilifu wa maisha, sisi ni mawakala ambao tunafanya kazi badala ya Mungu, tukisaidia kutekeleza mpango wa Mungu hapa na wakati huu. Na kwa wakati uleule, utimilifu wa maisha kwa milele ni lengo ambalo Mungu anamuita kila mmoja, sisi pia tunasaidia kuleta watu na viumbe vyote katika muungano mmoja katika Kristo ambapo hapo itakuwa nyumba yetu ya milele, mbinguni.

"Ukumbakumba wetu… Unaendeleza kazi ya Yesu ya kuleta wokovu Kwa kila kiumbe na Kuleta ukombozi Kutoka vitisho vyote Kwa utimilifu wa uzima."
Sheria # 5

Tupo makini KUWAPELEKA watu wote kwenye ukamilifu wa maisha. Tukitolea maisha yetu yote kwa ajili ya hilo, tunaitikia wito wa Mungu wa kumsaidia Mungu kutekeleza mpango wa wokovu. Zaidi ya hapo tupo makini pia kuona kwamba watu wote waweze kumjua Mungu kwa kutosha, kumpenda Mungu sana, na kujitoa wenyewe kwa Mungu bila kujibakiza. Jambo hili litatimilika kwa ukamilifu wake wa mbinguni, ambapo, kama ilivyoandikwa hapo juu, Mungu atakuwa yote katika yote. Kwa kutumia msemo wa Agustino "tutapumzika" (kwa kutosha na kwa ukamilifu) katika asili ya Mungu mwenyewe. Inaweza

ikaonekana hapa kwamba, katika hali Fulani, asili ya Mungu mwenyewe kuwa lengo la mwisho katika mpango wa ukombozi. Tumekuja kuishi kwa ajili ya Mungu, katika Mungu na kutukuza jina la Mungu milele. Katika injili ya Yohani, ambapo Yesu na Baba ni wamoja, Yesu Kristo, Mwokozi wetu, atakuwa ni lengo la mwisho wa mpango wa ukombozi. Alisema,"…Nitakaponyanyuliwa juu kutoka katika uso wa dunia, nitawavutia wote kwangu." (Yoh. 12:32) Sisi, waokolewa, tutajumuishwa wote katika fumbo la mwili wa Kristo (1kor12:12-27) na kwa pamoja tunafanya nafsi hiyo ambaye ni Kristo katika umbile lake kamili (Efe. 4:13)

KUSOMA UNDANI WA ALAMA ZA NYAKATI

Sisi Wasalvatoriani tunaitwa "kusoma alama za nyakati,"[vii] (Rejea *Gaudium et Spes*, No. 4) na kutenda inavyotakiwa, ili huduma zetu ziweze kuzaa matunda mengi. Hadithi nyingi mpya ulimwenguni zinalalamikia juu ya lengo letu. Tunaweza tukajimaliza kwa kuwasikiliza ili kutafuta alama za nyakati. Kama jambo hili lilivyo la manufaa mara nyingine alama za nyakati zilizo za muhimu sana zinatunzwa kwa ukimya ndani ya mioyo ya watu na akilini. Fikiria juu ya jambo hili: baadhi ya watu husema, "ninamwamini Mungu," au "ninamwamini Yesu,"lakini anasali kwa nadra na anakuja kanisani mara chache mno. Upendo wao uko wapi kwa Ekaristi? Kwa neno la Mungu ambalo linastawisha na kutoa uzima? Kwa kanisa katoliki? Baadhi ya watu wana wasiwasi kwa mficho ya kwamba wataenda motoni, na matumaini yao yaliyojificha ni kwamba watapata hukumu na kuingia mbinguni. Wanasumbuliwa na uhusiano usio wa uhakika na Mungu, ambaye yeye ni ukamilifu wa haki na mwingi wa huruma, maarifa na mwingi wa mapendo kwa uhakika atawatoa katika lawama ya mateso na kuwaruhusu waingie mbinguni bila kufuata utaratibu wa hukumu. Bado wapo pia wanaokiri imani yao kwa wasiwasi, na kusali kwa bidii sana, bila kujua vipi wampende Mungu kama rafiki yao. Kama mambo haya na mawazo mengine yanatawala katika akili na mioyo ya Wakristo, walio imara na dhaifu, kitu gani kinachotawala mioyo na akili ya wasio – Wakiristo? Baadhi wanamwini Allah na Nabii wake Mohammed, lakini wanamchukulia Kristo kwa heshima ya hali ya chini sana, kama iko hivyo kiuhalisia. Baadhi wanaamini mafundisho ya Buddha, na wengine wanamuheshimu sana Buddha. Ndugu zetu Wayahudi wanakubali Biblia yote ya Kiebrania, lakini sio Biblia ya Kikristo. Orodha nyingine ya, imani ya wasio Wakiristo ni ndefu na inatofautiana ulimwenguni kote! Tunawafikia vipi watu hawa na Habari Njema Tunawapasha vipi juu ya Yesu Kristo? Yeye ni baadhi ya alama za "kimya" ingawa ya ujumbe unaookoa yetu. Katika mioyo Aliyesulubiwa? Hizi Mkiristo, Mkiristo wa nyakati zilizo Mkiristo, anastahili zinagusa karama kamili. Kwa siri, yao, kila mtu, wokovu ni nini? Na, je, zamani, na asiye Kwa kutojua kabisa, umakini wetu ulio na wazo lolote juu ya wanaweza kutuuliza: wetu anayetupenda; ya nitaweza kuokolewa? ya nguvu ya Roho wanaweza kutokuwa Mungu, Muumba Yesu, Mwokozi, au Mtakatifu.

"Roho yetu ya ukumbakumba…tunajiweka wazi sisi wenyewe katika maswali na changamoto za kipindi chetu cha historia, kwa kuruhusu alama za nyakati kutufunulia njia na jinsi ya kuendana nazo."

Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani# 8a

Baba Fransis Jordani na Mama Maria wa Mitume walitunza kwa umakini mkubwa yale yaliyokuwa yanaendelea ndani ya akili na mioyo ya watu. Kama mfuasi wa Kristo, na kujisikia ameitwa kweli na Mungu kuanzisha shirika ambalo litashirikishana na Mungu kwa ajili ya wokovu

wa roho, Baba Jordani alianzisha kundi la watu: wanaume na wanawake walei, masista, mabruda na mapadre, kufanya kazi pamoja kama timu na kwenda ulimwenguni kama mitume, kuhuisha watu wote kuja katika imani kubwa na iliyojaa – mapendo katika Yesu Kristo mwana wa Mungu, na mwokozi wetu. Mitume hawa wangeweza kupata mahali ambapo watu walipo "kutoka ndani" na kufanya kazi kwa shauku, kwa moyo, kwa faida, na mara nyingine kwa uchangamfu kusahihisha makosa na kuweka ukweli wa Mungu badala yake. Mungu angeweza kuwaongoza, kama wangekuwa tayari kwa neno, kwa uelewa mpya na ulio dhahiri wa Mungu, maisha ya halafu, mbingu, jehanamu, mpango wa Mungu, msamaha wa Mungu, kanisa la Kristo, masakramenti kama msaada wa Mungu – ambao tumepewa kutokana na upendo, n.k.

Tunafuata mfano na uongozi wa Baba Jordani na wa Mama Maria wa Mitume kutangaza kwamba, licha ya wasiwasi imekuwa kinyume chake, na licha ya woga wote, Yesu Kristo ni kweli "njia na ukweli na uzima. Hakuna anayekuja kwa Baba isipokuwa kupita kwa [Yesu]." (Yoh 14:6) Kuhakikishiwa juu ya ukamilifu wa uzima mbinguni, Yesu mwenyewe ni njia, chanzo cha kweli cha uzima na uzima wenyewe wa Mungu.

WOKOVU: KUWAONGOZA WENGINE KWENYE UHURU, SEHEMU ZA WAZI

Wokovu upo pia katika mtindo mwingine: ule wa kuwaongoza watu kwenye uhuru, katika sehemu za wazi. Ingawa mtindo huu ulikuwa unapendwa sana katika miaka ya 1970, lakini bado ni mashuhuri. Mtindo huu unaona ya kwamba tendo la Wokovu wa Mungu kwa Wayahudi waliokuwa utumwani Misri. Maisha yao yalikuwa ni ya mateso na maumivu, "yakiambatana na kazi ngumu za ujenzi na ufyatuaji wa matofali na aina zote za kazi za shamba – ambao ni ukatili wote wa majanga ya watumwa." (Kut 1:14). Kutoka katika mateso yao, Mungu aliwakomboa! Mungu aliwatoa kutoka katika nchi ya Misri kwa miujiza, wakiongozwa na Musa mtumishi wake. Sisi Wasalvatoriani tunaitwa pia kuwasaidia kuwaongoza watu kutoka katika jela na magereza yao, kutoka katika pingu zao na minyororo. Inabidi tuwakomboe kutoka katika hofu zao za ndani na maumivu na mateso yao ya nje. Tunatakiwa tuponye vidonda vyao, kuwapa msaada wa kiafya, na kuwapa maji safi ya kunywa. Tunatakiwa tuwafute machozi yao na kuwa kitu ambacho kitaweza kuwafanya watabasamu, kama Mungu-akipenda. Tunatakiwa tumwombe Mwokozi wetu atusaidie tuwafikishe katika nchi ya ahadi ya amani na kuridhika, ya furaha na matumaini. Hii pia, ni uzima tele ambao Yesu aliahidi.

YESU KRISTO: MWANZO NA MWISHO

Yesu Kristo ni Uzima Wenyewe… na pia ni uzima uliokamilika. Kama sisi Wasalvatoriani tunahitaji kuwa na teolojia yoyote ya wokovu kwa namna yoyote ile, ngoja tumalize na wazo hilo. Mwokozi ambaye anaongoza njia yetu, mtoto mchanga ambaye alichukuwa mwili wetu wa kibinadamu, kijana mwenye akili na anayeuliza maswali makubwa, muhubiri, rafiki wa mbatizaji, jalimu, mponyaji, mlisha kundi kubwa la wenye njaa, rafiki wa waliobaguliwa, wadhambi, wanawake, watoto, waliodhulumiwa, fukara, maskini, mtumishi anayeteseka, msulubiwa, bwana mfufuka, bwana wa mitume, mwana wa Maria…yeye ni uzima wa milele. Mambo yote tunayoweza kusema juu ya wokovu yataishia kwake. Yeye ni mwanzo na mwisho, Alpha na Omega. (Rej. Ufu 1:8), Kristo, Uzima Wetu, Uje Utuokoe!

Maswali ya Tafakari

1. Soma tena Sheria za Familia ya Kisalvatoriani kwa mwanga wa makala hii.
    a. Onyesha maneno au misemo ambayo inakugusa na ujiulize, "jambo hili linaniambia mimi nini na nitalipa mwitikio gani?"
    b. Manufaa yake yanaweza kuwa ni yapi katika familia ya Kisalvatoriani katika eneo lako la ulimwengu au/na kwa ulimwengu mzima?
2. Kwa mwanga wa makala hii, kama ukiamua kuitengeneza upya sheria ya familia ya Wasalvatoriani, Je, Utaongeza kitu gani au kukibadili?
3. Mwandishi anaandika kuhusu alama za ndani za nyakati kama maswali yanayotoka kutoka katika mioyo ya watu. Kwa upande wako maswali ya ndani ni yapi; kwa wale unaowahudumia au na wale ambao mnafanya nao utume? Majibu gani yanayotoka kutoka karama yetu ya wasalvatoriani ambayo ungeweza kutoa; utakayoyatoa?

---

i

ii

iii

iv

v

vi

vii